# Kulikuwa na Hila za Da Vinci?

## Tabasamu la MonaLisa

*Maandiko ya Da Vinci* si ya kudharauliwa kama mpango wa hila za kutunga. Kauli yake kwamba Yesu Kristo amepikwa kwa madhumuni ya kisiasa, inahatarisha msingi hasa wa Ukristu. Mtunzi wake, Dan Brown, amesema katika TV ya Taifa kwamba, hata kama mpango ni wa kutunga, anaamini maelezo ya wasifu wa Yesu ni ya kweli. Kwa hiyo upi ni ukweli? Hebu tuangalie.

- Je Yesu alikuwa na ndoa ya siri na Mary Magdalene?
- Je, Utakatifu wa Yesu ulipangwa na Constantine na kanisa?
- Je, kumbukumbu halisi za Yesu ziliharibiwa?
- Je, maandishi yaliyogunduliwa hivi karibuni yanasema kweli kuhusu Yesu?

Je, hila kuu zimeleteleza kubuniwa kwa Yesu? Kulingana na kitabu na sinema, *Maneno ya Da Vinci*, hivyo ndivyo ilivyotokea hasa. Madai kadhaa ya vitabu kuhusu mwashirio wa hila kwa Yesu. Kwa mfano, kitabu kinasema:

> "Hakuna mtu anayesema Kristo alikuwa mwongo, wala anayekana kwamba Yesu alitembea duniani na aliwafanya mamilioni kuwa na maisha bora. Yote tunayosema ni kwamba ConstantiAne alijipatia nafasi kupitia umaarufu mkubwa na umuhimu wa Yesu. Na kwa kufanya hivyo, alitengeneza sura ya Ukristo kama tunavyoujua."[1]

Ingewezekana madai haya ya kushangaza toka kwa katika kitabu kiuzwacho sana cha Dan Brown kuwa kweli? Au lengo nyuma yake ni habari tu ya hadithi ya hila nzuri sawa na imani kwamba wageni walidondokea Roswell, New Mexico, au kulikuwa na mshika-mtutu wa pili kwenye kilima cha majani Dallas wakati JFK alipouawa? Kwa vyovyote vile, hadithi inavutia.

Hakuna maajabu kwamba kitabu cha Brown kimekuwa ni kimojawapo cha hadithi zilizouzika sana katika mwongo (kipindi cha miaka kumi)

## Hila za Yesu

*Siri za Da Vinci* zinaanza na mauaji ya mtunza nyumba ya makumbusho aliyeitwa Jacques Sauniere Profesa msomi wa Harvard na mwandishi mzuri wa maandiko ya siri wa Ufaransa wanapewa kazi ya kufumbua ujumbe ulioachwa na mtunza nyumba ya makumbusho kabla ya kifo chake. Ujumbe unafunuliwa kuweka wazi hila kubwa katika historia ya wanadamu; kufichwa kwa ujumbe wa kweli wa Yesu Kristo na mamlaka ya siri ya Kanisa Katoliki la Roma iliyoitwa Opus Dei.

Kabla ya kifo chake, mtunza makumbusho alikuwa na ushahidi ambao ungeweza kukanusha utakatifu wa Kristo. Japokuwa (kulingana na hila) kanisa limejaribu kwa karne kuzima ushahidi, wafikiriaji wakubwa na wasanii wamepandikiza siri kila mahali: katika michoro kama vile *Mona Lisa* na *Karamu ya Mwisho* na Da Vinci, katika majengo ya makanisa, hata katika katuni za Disney. Madai makubwa ya kitabu ni haya:

- Mtawala wa Kirumi Constantini alishiriki kumfanya Yesu Kristo kuwa Mungu.
- Constantini binafsi alichagua vitabu vya Agano Jipya.
- Injili za Kiroho zilikatazwa na wanaume kuwakandamiza wanawake.
- Yesu na Maria Magdalena walioana kwa siri na walikuwa na mtoto.
- Maelfu ya nyaraka za siri zinakanusha hoja muhimu za Ukristu.

Brown aweka wazi hila zake kupitia mtaalamu wa vitabu vya kutunga, mwanahistoria wa koo za kifalme wa Uingereza Sir Leigh Teabing. Akidhihirishwa kama msomi mwenye busara wa kale, Teabing anaweka wazi kwa mwandishi-visiri (maandiko ya siri) Sophie Neveu kwamba katika Halmashauri ya Nicaea a.d. 325 "vipengele vingi vya ukristu vilijadiliwa na kupigiwa kura" kikiwemo cha utakatifu wa Yesu.

> “Hadi wakati huo katika historia,” anasema “Yesu alionekana na wafuasi wake kama mtume mkuu… mtu mkuu mwenye nguvu, lakini ni mwenye nguvu licha ya kuwa binadamu”
>
> Neveu anashtushwa. “Si Mwana wa Mungu?” anauliza.Teabing anaeleza: “Madai ya Yesu kama ‘Mwana wa Mungu’ yalipendekezwa rasmi na kupigiwa kura na Halmashauri ya Nicaea.”
>
> “Subiri. Unasema utakatifu wa Yesu ulikuwa ni matokeo ya kura?”
>
> “Kura ya karibu katika” Teabing anamweleza mwandishi visiri aliyeshangazwa.”[2]

Kwa hiyo, kulingana na Teabing, Yesu hakuchukuliwa kama Mungu hadi Halmashauri ya Nicaea kipindi cha a.d. 325, je ni lini kumbukumbu halisi za Yesu zinasadikiwa kupigwa marufuku au ziliharibiwa?

Hivyo, kulingana na nadharia, msingi mzima wa Ukristu umewekwa kwenye uongo. *Siri za Da Vinci* zimeuza hadithi yake vizuri, zikivuta mapendekezo toka kwa wasomaji kama vile “Ikiwa haikuwa kweli, isingechapishwa!” Mwingine alisema “hangetia mguu kanisani tena.” “Mrejea wa Kitabu alikisifu kwa utafiti wake makini kamilifu usio na dosari.”[3] Ushawishi mzuri kwa kazi kutunga.

Wacha tukubali kwa muda kwamba mapendekezo ya Teabing yanaweza kuwa kweli. Kwanini kwa hali hiyo Halmashauri ya Nicaea iliamua kumtukuza Yesu kwa utakatifu?

“Ilikuwa hivyo kwa ajili ya mamlaka, ” Teabing anaendelea. “Kristo kama Masiya alikuwa muhimu kwa utendajikazi wa Kanisa na nchi. Wanafunzi wengi wanadai kwamba Kanisa la kwanza kwa kweli lilimwiba Yesu kutoka kwa wafuasi wake halisi, likiteka taarifa zake za kibinadamu, likazificha ndani ya la vazi la dini, na likazitumia kupanua mamlaka yake.”[4]

Kwa namna nyingi, *Maandishi ya Da Vinci* ni nadharia ya mwisho ya kushiriki hila Ikiwa madai ya Brown ni sahihi, basi tumekuwa tukidanganywa na kanisa, na historia na Biblia. Labda hata na hao tuwaaminio zaidi: wazazi wetu au walimu wetu. Na yote yalikuwa ni kwa ajili ya kutwaa mamlaka.

Ingawaje *Siri za Da Vinci* ni za kutunga, hazijengi sana dhana yake kwenye matukio ya kweli (Halmashauri ya Nicaea), watu halisi (Constantine na Arius), na nyaraka halisi (Injili za Kiroho). Ikiwa tunapaswa kujua kwa kina kuhusu hila hizi, kazi yetu ni lazima kushughulikia madai ya Brown na kutengananisha ukweli mbali na kutunga.

## Constantine na Ukristo

Katika karne kabla ya utawala wa Constantini kwa Kimaya ya Kirumi, wakristu walikuwa wakiteswa sana. Lakini pia, wakati akijiimarisha katika vita, Constantine aliripoti kuwa ameona nuru angavu ya msalaba angani iliyochorwa na maneno “Shinda kwa hii.” Aliingia katika mapambano chini ya ishara ya msalaba na alichukua utawala himaya.

Kubadili kwa wazi kwa Constantine kuingia Ukristu kulikuwa ndio eneo kutofautiana katika historia ya kanisa. Roma ikawa ni himaya ya Kikristo. Kwa mara ya kwanza kwa karibu miaka 30, ikawa salama kiasi, na safi kuwa mkristo.

Wakristu hawakuteswa tena kwa imani yao. Constantini kisha akatafuta kuunganisha Himaya za Mashariki na Magharibi ambazo ziligawanywa vibaya kwa itikadi, imani, taratibu, akaleta habari ya utambulisho wa Yesu Kristo.

Hizi ni baadhi baadhi ya vyombo vya ukweli katika *Siri za Da Vinci*,na vyombo vya ukweli ni utangulizi kwa wazo lolote la hila za mafanikio. Lakini hila za kitabu zinamgeuza Constantine kuwa mshiriki-hila. Kwa hiyo tushughulikie suala muhimu la msingi lililoletwa na nadharia ya Brown; je Constantine ndiye alivumbua imani wa kikristo ya utakatifu wa Yesu?

## Kumtukuza Yesu

Ili kujibu madai ya Brown, lazima kwanza tutambue kitu gani wakristo kwa ujumla waliamini kabla Constantine

hajaitisha mkutano wa Halmashauri ya Nicaea.

Wakristu wamekuwa wakimwabudu Yesu kama Mungu tangu karne ya kwanza. Lakini katika karne ya nne, kiongozi wa kanisa kutoka mashariki, Arius, alianzisha kampeni kulinda utakatifu-mmoja wa Mungu. Alifundisha kwamba Yesu aliumbwa mahususi mkuu kuliko malaika, lakini si Mungu. Athanazi na viongozi wakuu wa kanisa kwa upande mwingine, walisadikishwa kwamba Yesu alikuwa ni Mungu katika mwili.

Constantine alitaka kusuluhisha mzozo huo, akitumaini kuleta amani katika himaya yake, akiunganisha migawanyiko ya mashariki na magharibi. Hivyo mwaka 325 A.D., aliita zaidi ya maaskofu 300 katika Nicaea (ambayo kwa sasa ni sehemu ya Uturuki) toka katika dunia yote ya Ukristu. Suala nyeti ni, je kanisa la mwanzo lilifikiria Yesu alikuwa Muumbaji au tu ni uumbaji – mwana wa Mungu au mwana wa mseremala? Hivyo, ni kitu gani manabii walifundisha kuhusu Yesu? Kutoka katika kauli za mwanzo kabisa zilizorekodiwa, zilimchukulia kama Mungu. Karibu miaka 30 baada ya kifo na ufufuko wa Yesu, Paulo aliandika kwa Wafilipi kwamba Yesu alikuwa ni Mungu katika umbo la kibinadamu (Wafilipi 2:6-7, NLT). Na Yohana, shahidi wa macho wa karibu, anahakikisha utakatifu wa Yesu katika kifungu kifuatacho:

> Hapo mwanzo Neno tayari lilikuwapo. Alikuwa na Mungu, na alikuwa Mungu. Aliumba kila kitu hapo kilipo Hakuna chochote kilichopo ambacho hakukiumba. Uhai/Maisha yenyewe yalikuwa ndani yake, hivyo Neno akawa mwanadamu na akaishi hapa duniani kwetu sisi (Yohana 1: 1-4, 14, NLT).

Kifungu toka kwa Yohana 1, kimevumbuliwa katika maandishi ya kale, na kimewekewa tarehe ya kaboni mnamo 175-225 A.D. Hivyo Yesu kwa uwazi alizungumziwa kama Mungu zaidi ya miaka mia moja kabla ya Constantine hajaitisha mkutano na Baraza la Nicaea. Sasa tunaona kwamba ushahidi wa maandishi wa kisayansi unapinga madai ya maandishi ya Da Vinci kwamba Utakatifu wa Yesu ulikuwa ni uvumbuzi wa karne ya nne. Lakini nini historia inatuambia kuhusu Baraza la Nicaea? Brown anadai katika kitabu chake kupitia kwa Teabing, kwamba wengi wa maaskofu Nicaea walilazimisha imani ya Arius kwamba Yesu alikuwa "mtume wa siku zote" na wakachukua imani ya utakatifu wa Yesu kwa kura ya karibu kiasi." Uongo au kweli?

Kwa ukweli, kura ilikuwa ya ushindi mkubwa; wawili tu kati ya maaskofu 318 walipinga. Ambapo Arius aliamini kwamba Baba peke yake alikuwa Mungu, na kwamba Yesu alikuwa kiumbe chake kikuuu, Baraza lilihitimisha kwamba Yesu na Baba walikuwa wa asili sawa ya utakatifu mtakatifu.

Baba na Mwana na Roho Mtakatifu walionekana kuwatofauti, walikuwa pamoja, wadumuo milele kwa pamoja, lakini Mungu mmoja. Imani ya Mungu mmoja katika nafsi tatu ikapata kujulikana kama imani ya Nicene, na ni msingi mkuu wa Imani ya Kikristo. Sasa, si kweli kwamba Arius alikuwa mshawishi na alikuwa na ushawishi mkubwa. Kura ya ushindi mkubwa ikafuatia baada ya majadiliano mazito. Lakini mwishoni mwa Baraza kwa kushinda kwa nguvu likatangaza Arius kuwa mpinzani kwa sababu mafundisho yake yanapingana na kile mitume walikuwa wakifundisha kuhusu utakatifu wa Yesu.

Historia pia inakikisha kwamba Yesu aliruhusu kwa waziwazi kuheshimiwa alikopokea toka kwa wafuasi wake. Na, kama tulivyoona, Paulo na mitume wengine kwa wazi walifundisha kwamba Yesu ni Mungu na anastahili kuabudiwa.

Tangu siku za kwanza za Kanisa la Kikristo, Yesu alichukuliwa zaidi ya mtu wa kawaida, na wengi wa wafuasi wake walimwabudu yeye kama Bwana-Muumbaji wa ulimwengu. Hivyo, jinsi gani Constantine awe amebuni imani ya utakatifu wa Yesu ikiwa kanisa lilishamchukulia Yesu kama Mungu kwa zaidi ya miaka 200? Maandiko ya *Da Vinci hayaelezei* suala hili.

## Kushambulia Kitabu cha Dini

*Maandishi ya Da Vinci* pia yanaeleza kwamba Constantine alikandamiza/ficha maandiko yote yamhusuyo Yesu zaidi ya hayo yaliyopatikana katika Agano Jipya letu la sasa (yaliyotambuliwa na kanisa kama ripoti za ushahidi halisi wa macho za mitume. Inadaiwa zaidi kwamba maelezo ya Agano Jipya yalibadilishwa na Constantine na maaskofu kumwelezea Yesu upya. Suala lingine la msingi la*la ushiriki wa maandiko ya Da Vinci* ni kwamba injili

nne za Agano Jipya ziliteuliwa toka katika jumla ya zaidi ya injili 80, nyingi kati ya hizo inasadikiwa zilifichwa na Constantine.[5]

Kuna masuala makuu mawili hapa, na tunahitaji kuyashughulikia yote.  La kwanza ni kwamba je Constantini alibadilisha au alipendelea uteuzi wa Vitabu vya Agano Jipya. La pili ni kwamba alizuia maandiko ambayo yangejumuishwa katika Biblia.

Tukitazama suala la kwanza, barua na maandiko yaliyoandikwa na viongozi wa kanisa wa karne ya pili na wapinzani vile vile wanahakikisha matumizi makubwa ya vitabu vya Agano Jipya. Karibu miaka 200 kabla ya Constantine hajaita Baraza la Nicaea, mpinzani Masioni aliorodesha 11 kati ya 27 ya vitabu vya Agano jipya kama maandiko halisi ya mitume.

Na karibia wakati huo huo, mpinzani mwingine, Valentinus, anagusia katika aina nyingi mbali mbali za vifungu na ujumbe wa Agano Jipya. Kwa sababu wapinzani wawili walikuwa wapinzani uongozi wa kanisa wa zamani za mwanzo, hakuwa wanaandika kile maaskofu walitaka. Lakini kama ilivyokuwa kwa kanisa la kale, bado walirejelea katika vitabu vya Agano Jipya tusomavyo leo.

Hivyo, ikiwa Agano Jipya tayari lilikuwa katika matumizi miaka 200 kabla ya Constantine na Baraza la Nicaea, ni jinsi gani mtawala angeweza kulibuni na kulibadili? Kabla ya wakati huo kanisa lilikuwa limeshaenea na kukusanya mamia ya maelfu kama siyo mamilioni ya waamini, wote walikuwa wanafahamu maelezo ya Agano Jipya.

Katika kitabu chake, *Ulaghai wa Da Vinci,*, upembuzi wa *Maandishi ya Da Vinci,* Dk. Erwin Lutzer anasema,

> “Constantine hakuamua vitabu gani viwemo katika orodha rasmi ya dini, pia mada ya orodha rasmi ya vitabu vya dini haikujitokeza katika Baraza la Nicaea. Kabla ya wakati huo, kanisa lilikuwa likisoma orodha rasmi ya vitabu vya dini ambayo ilikuwa imehakikisha ilikuwa ni Neno la Mungu miaka mia mbili kabla.”[6]

Ingawaje orodha rasmi ilikuwa bado miaka kabla haijahitimishwa, Agano Jipya la leo lilionekana rasmi zaidi ya karne mbili kabla ya Nicaea.

Hii inatuleta kwenye suala la pili; kwani injili hizi za kiroho za siri ziliharibiwa na kuondolewa toka katika Agano Jipya? Ndani ya kitabu, Teabing anadai kwamba maandiko ya siri yaliondolewa toka katika Biblia 50 zilizoidhinishwa ikisimamiwa na Constantine katika Baraza. Alimwambia Neveu kwa shauku:

> “Kwa sababu Constantine alikweza hadhi ya Yesu karibia karne nne baada ya Kifo cha Yesu, maelfu ya maandiko tayari yalikuwapo yakiandika maisha yake kama mtu tu. Kuandika tena historia ya vitabu, Constantine alijua angehitaji kitendo cha kishujaa. Kutoka katika hili pakajitokeza wakati muhimu katika historia ya Kikristo.”[7]

Constantine akaamuru na akafadhili Biblia mpya ambayo iliondoa hizo injili ambazo zilizungumzia sifa/tabia pambanishi za kibinadamu za Kristo na akapamba injili hizo ambazo zilimfanya yeye kama Mungu.  Injili za mwanzo zilitanguliwa, zikakusanywa na zikachomwa moto.

Je, haya maandiko ya wachache ya siri yalikuwa ni historia ya kweli ya Yesu Kristo? Ngoja tuangalie kwa kina tuone kama tunaweza tenganisha ukweli kutoka kwa kubuni.

#### “Wajuaji” wa siri

Injili za siri za wachache zinaunganishwa kwenye kundi lijulikanalo kama (shangazo kuu hapa) Elimu ya Siri. Jina lao linatoka katika neno la kigiriki, *gnosis*, likimaanisha “maarifa” Watu hawa walifikiri wana siri, maarifa maalumu yaliyofichwa mbali na watu wa kawaida.

Kati ya maandiko 52, matano tu yaliorodheshwa kama injili. Kama tutakavyoona, hizi ziitwazo injili zinatofautishwa toka katika Injili za Agano Jipua, Mathayo, Mark, Luka na Yohana.

Kama Ukristu ulivyoenea, ujuzi ulichanganya baadhi ya imani na masuala ya ukristu katika imani zao wakichanganya ujuzi kwenye Ukristu bandia. Labda walifanya hivyo kuongeza idadi ya kuajiri na kumfanya Yesu mtoto wa matangazo kwa sababu zao. Pia, ili utaratibu wao wa fikra uweze kuendana na Ukristu, Yesu alihitaji kuwa kuelezewa upya, akavuliwa wote ubinadamu wake na utakatifu wake halisi.

Katika *Historia ya Ukristu ya Oxford*, John McManners aliandika mchanganyiko wa elimu siri wa ukristu na imani za kubuni za uongo.

> "Ujuzi-siri ulikuwa (na bado ni) theosophia (elimu ya Mungu ya kiroho) zenye michanganyiko mingi. Ushirikina na imani za uongo za kienyeji zilichanganywa na elimu ya nyota, uchawi. … wakakusanya misemo ya Yesu iliyotengenezwa kufaa tafsiri zao (kama katika Injili ya Thomaso), na wakawapa wafuasi wao fursa au namna ya upinzani wa Ukristu ."[8]

## Kosozi za mwanzo

Kinyume na madai ya Brown, haikuwa Constantine aliyefanya imani za Kinostiki(Imani ya Uficho) kuwa pinzani; ilikuwa ni mitume wenyewe. Mazoea kidogo yaa falsalfa yalikuwa tayari yanakua katika karne ya kwanza, miongo kadhaa ya kifo cha Yesu.. Mitume katika mafundisho na maandiko yako, walienda mbali kulaumu imani hizi kwamba zimepingana na ukweli wa Yesu, kwake yeye ambaye walikuwa mashahidi wa macho.

Angalia, kwa mfano, kile mtume Yohana aliandika karibu mwisho wa karne ya kwanza:

> "Nani ni mwongo mkubwa"? Anayesema kwamba Yesu si Kristo. Watu hao ni wapinga Kristo, kwa sababu wamemkana Baba na Mwana." (1 Yohana 2:22)

Likifuata mafundisho ya mitume, viongozi wa kanisa la mwanzo kwa pamoja wakalaumu mafundisho ya Kinostiki ya siri ya wachache kuwa ni kidhehebu-tenge. Padri wa Kanisa Irenaeus, akiandika miaka 140 kabla ya Baraza la Nicaea, alihakikisha kwamba Wanostiki walilaumiwa na kanisa kama wapinzani. Pia alizikataa "injili" zao. Vile vile, akirejelea kwenye Injili nne za Agano Jipya, alisema, "Haiwezekani kwamba Injili zinaweza kuwa zaidi au chache katika idadi kuliko zilivyo." [9]

Mwanateolojia Origen aliandika hili katika karne ya tatu, zaidi ya miaka mia moja kabla ya Nicaea:

> Najua injili fulani ambayo inaitwa "Injili kulingana na Thomaso" na "Injili kulingana na Mathayo", na nyingi nyinginezo tulizosoma – tusifikiriwe kwa njia yoyote wajinga kwa sababu ya hao wanaofikiri wanamiliki elimu fulani ikiwa wamejulishwa haya. Hata hivyo, miongoni mwa yote haya tuliyothibitisha pekee ambayo kanisa limetambua, ambalo ni kwamba Injili nne tu zinapaswa kukubaliwa.[10]

Hapo tunayo katika maneno ya kiongozi wa kanisa anayeheshimiwa sana. Wanostika (Wenye Elimu-Ficho) walitambuliwa kama dhehebu lisilo la kikristo barabara kabla ya Baraza la Nicaea. Lakini kuna ushahidi zaidi unauliza madai yaliyofanywa katika *Maandiko ya Da Vinci*.

## Nani ni mbaguzi wa kijinsia?

Brown anapendekeza kwamba mojawapo ya vichocheo kwa ajili ya kupiga marukufu maandishi ya kinostiki (ya wachache) na Constantine kunakosemekana ilikuwa ni tamaa ya kukandamiza wanawake katika kanisa. Kinyume chake kikejeli, ni Injili baguzi ya Thomas ambayo inadhalilisha wanawake . Inahitimisha (kulingana na hali ikimnukuu Peter) pamoja na kauli hii ya kushangaza: "Mwacheni Maria aende mbali nasi, kwa sababu wanawake hawana thamani na maisha" (114).[11] Kisha Yesu kama inavyodaiwa akamwambia Petro atamfanya Maria awe

mwanamme ili aweze kuingia katika ufalme wa mbinguni. Soma: wanawake ni duni. Kwa fikira kama hizo zinazooneshwa, ni vigumu kuelewa maandiko ya Kinostiki ya wabaguzi wachache kuwa ni mapambano kwa ajili ya kuwakomboa wanawake.

Kwa kinyume kabisa, Yesu wa injili za Kibiblia siku zote amekuwa akiwatendea wanawake kwa utu na heshima. Aya endelevu za kimageuzi kama hii mojawapo ndani ya Agano jipya zimekuwa ni msingi kwa majaribio katika kuinua hadhi ya wanawake:

> "Hakuna tena myahudi au mtaifa, mtumwa au mtu huru, mwanamme au mwanamke. Kwenu ninyi wakristu- ninyi ni wamoja katika Kristo Yesu" (Wagalatia 3:28, NLT).

**Watunzi wa Siri**

Inapokuja kwenye injili za kibaguzi, karibu kila kitabu kinabeba jina la sifa ya Agano Jipya: Injili ya Philipo, Injili ya Petro, Injili ya Maria, Injili ya Yuda, na kuendelea . (Vinakuwa kama orodha ya majina katika shule ya parokia.) Hivi ni vitabu ambavyo nadharia ya ushiriki kula hila kama *Maandiko ya Da Vinci* yanajikita. Lakini ziliandikwa na watunzi wao waliokusudiwa?

Injili za Kibaguzi zinawekewa tarehe karibia miaka 100 hadi 300 baada ya Kristo, hakuna msomi wa kuaminika anaamini chochote kati ya hivyo ambavyo vingeweza kuandikwa na wenzi-jina (somo) wao. Katika maktaba ya James M. Robinson's *Maktaba ya Nag Hammadi* , tunajivunza kwamba Injili za kibaguzi ziliandiwa hasa kwa kiasi kikubwa na watunzi wasiojulikana wasiohusiana." [12] Dr. Darell L. Bock, profesa wa masomo ya Agano Jipya katika seminari ya Theolojia ya Dallas, aliandika,

> "Sehemu kubwa ya maandishi haya ni vizazi vichache viliondolewa toka katika misingi ya imani ya kikristu, pointi muhimu kukumbuka wakati wa kutathmini mada ziliyomo."[13]

Msomi wa Agano Jipya Norman Geisler alitoa maoni kwa maandiko mawili ya kibaguzi, Injili ya Peter na Matendo, ya Yohana. (Maandiko haya ya Kibaguzi yasichanganywe na vitabu vya Agano Jipya vilivyoandikwa na Yohana na Petro):

> "Maandiko ya Kibaguzi hayakuandikwa na mitume, isipokuwa watu wengine katika karne ya pili (na baadaye) wakijifanya kutumia mamlaka ya kitume kuendeleza mafundisho yao wenyewe. Leo tunaita suala hili uongo na uzushi-gushi."[14]

Injili za Kinostika (Kibaguzi) si maelezo ya kihistoria ya maisha ya Yesu bali badala yake ni maneno ya wachache, yaliyofichwa katika fumbo-siri, yakiacha maelezo ya kihistoria kama majina, sehemu na matukio. . Hii ni kinyume kabisa na Injili za Agano Jipya ambazo zimekusanya maelezo ya kweli yasiyo na idadi kuhusu maisha ya Yesu, idara na maneno.

## Bi Yesu

Sehemu ya kuchekesha zaidi ya hila za Da Vinci ni madai kwamba Yesu na Maria Magdalene walikuwa na ndoa ya siri ambayo ilizaa mtoto kuendeleza kizazi chake. Zaidi ya hayo, tumbo la Maria Magdalene's, linalobeba kitoto cha Yesu, inaelezwa katika kitabu kama kikombe kitakatifu maarufu, siri inayoshikiliwa na Shirika Katoliki liitwalo Utawa wa Sayuni. Bw. Isaac Newton, Botticelli, Victor Hugo na Leonardo Da Vinci wote walinukuliwa kama wanachama.

Mapenzi Kashifa Kula hila. Jambo kubwa kwa fikra ya kushiriki hila Lakini ni kweli? Hebu tuangalie kile wasomi wanasema.

A *makala ya Gazeli la Newsweek* ambayo ilifupisha maoni ya wanafunzi, ilihitimisha kwamba nadharia kwamba

Yesu na Maria Magdalena walikuwa wameoana kwa siri haina msingi kihistoria.[15] Pendekezo lililoletwa mbele katika *Maandiko ya Da Vinci* imejengwa kwenye aya pekee katika Injili ya Philipo ambayo inaonesha Yesu na Maria walikuwa washirika. Katika kitabu, Teabing anajaribu kujenga dhana kwamba neno washirika lingemaanisha wanandoa! Lakini nadharia ya Teabing haikubaliwi na wanafunzi.

Pia kuna mstari pekee katika Injili ya Philipo ambayo inasema Yesu alimbusu Maria. Kuwasalimia marafiki kwa busu kulikuwa kawaida katika karne ya kwanza, na hakukuwa na ishara ya mapenzi. Lakini hata kama*tafsiri ya Maandiko ya Da Vinci* ni sahihi, hakuna maandiko mengine ya kihistoria kuthibitisha nadharia yake. Na kwa sababu Injili ya Philipo ni maandiko yaliyogushiwa yaliyoandikwa miaka 150 hadi 220 baada ya Kristo na mwandishi asiyejulikana, maelezo yake kuhusu Yesu si ya uhakika kihistoria.

Labda Wanostika walifikiri Agano Jipya lilikuwa kidogo na aibu kuhusu mapenzi na wakaamua suala kuliongezea chumvi kidogo . Kwa sababu yoyote ile, aya ilitengwa na iliyojificha iliyoandikwa karne mbili baada ya Kristo si ya kuzingatilia nadharia ya hila juu yake. Inavutia kusoma labda, lakini hasa si historia.

Kama ilivyo kwa Kikombe Kitakatifu na Utawa wa Sayuni, maelezo ya kutunga ya Brown tena yanapotosha historia. Kikombe kitakatifu maarufu kilikuwa hasa Kikombe cha Yesu kwenye karamu yake ya mwisho na hakikukuwa na suala lolote kumhusu Mary Magdalena. Na Leonardo da Vinci hakujua kuhusu Utawa wa Sayuni, kwa sababu haikuasisiwa hadi 1956, miaka 437 baada ya kifo chake.. Pia, hadithi ya kuvutia, lakini ni historia feki bandia ya kutunga.

## Nyaraka za “siri”

Lakini vipi kuhusu maelezo ya Teabing kwamba “maelfu ya nyaraka za siri” zinathibitisha kwamba Ukristu ni uongo? Je ingeweza kuwa kweli?

Ikiwa kulikuwa na maandiko, wasomi waliopingwa kwa ukristu wangekuwa na siku ya kushughulika pamoja nao. Maandiko ya kugushi ambayo yalikataliwa na kanisa la mwanzo kwa maoni pinzani siyo siri, yamekuwa yakijulikana kwa karne. Hakuna cha kushangaza hapo. Hayajawahi kufikiriwa ni sehemu ya maandiko halisi ya mitume.

Na ikiwa Brown (Teabing) anagusia ripoti za mashaka, au Injili changa za mwanzo, pointi hiyo pia ipo nje ya mada. Si siri na wala hayakani Ukristu. Mwanafunzi wa Agano Jipya Raymond Brown amezungumzia Injili za Kibaguzi:

> “Tunajifunza si tu ukweli mpya pekee wa kuthibitika kuhusu idara ya Yesu ya kihistoria, na minong’ono michache ambayo inawezekana ikawa yake.”[16]

Si kama Injili za Wanostika wachache, ambao watunzi wake hawajulikani na hawakuwa mashahidi wa macho, Agano Jipya tulilo nalo leo limefaulu mitihani mingi ya uhalisia . (Andiko la Yesu) Hali ni ya kutisha kwa hao wanaong’ang’ania nadharia ya ushiriki wa hila Mwanahistoria wa Agano Jipya F.F. Bruce aliandika:

> “Hakuna mkusanyiko wa fasihi za kale duniani unaofaidi utajiri wa uthibitisho mzuri wa maandishi.”[17]

Mwanafunzi wa Agano Jipya Bruce Metzeger aliweka wazi kwanini Injili ya Thomaso haikukubaliwa na kanisa la kale:

> “Si sawa kusema kwamba Injili ya Thomaso iliondolewa na baadhi ya amri rasmi katika sehemu ya Baraza: njia sahihi ya kusema ni kwamba Injili ya Thomaso ilijiondoa yenyewe! Haikuendana na ushuhuda mwingine kuhusu Yesu kwamba wakristo wa kale waliukubali kama wenye thamani.”[18]

## Uamuzi wa Historia

Hivyo, ni kitu gani tunahitimisha kuhusu mawazo mbalimbali ya hila kuhusu Yesu? Karen King, profesa wa historia ya kanisa la kikristo Havard, ameandika vitabu kadhaa kuhusu Injili za Kibaguzi ikiwamo Injili ya Mary wa Magdala na Unostika(Ujuzi-baguzi) ni nini,? King, ingawaje ni wakili shupavu wa mafundisho ya wachache, alihitimisha :Mawazo haya kuhusu nadharia ya hila… ni mawazo finyu ambayo hayana msingi wa kihistoria."[19]

Licha ya kukosa ushahidi, nadharia za hila zitauza mamilioni ya vitabu na kuweka rekodi ya mauzo ya ofisi. Wanafunzi katika nyanja zinazohusiana, baadhi ya wakristu na wengine bila imani hata kidogo, wamebishia madai ya maandiko ya Da Vinci. Vilevile na dhamira zilizoyumba kwa urahisi bado zinashangaa; kunaweza kuwa na kitu fulani baada ya yote?

Mwandishi wa habari wa televisheni aliyeshinda tuzo, Frank Sesno aliuza kundi la wanafunzi wa kihistoria kuhusu kupumbazwa watu wamekuwa nao kuhusu nadharia za hila. Profesa Stanley Kutler toka Chuo Kikuu cha Wisconsin alijibu, "Wote tunapenda mafumbo na siri lakini tunapenda hila-hila zaidi."[20]

Hivyo, ikiwa unataka kusoma dhana kuu za hila-hila kuhusu Yesu, hadithi za Dan Brown's, Siri za Da Vinci, zinaweza kuwa ticket kwako. Lakini kama unataka kusoma maelezo ya Yesu Kristo, basi Mathayo, Marko, Luka na Yohana watakurejesha kwenye kile mashahidi wa macho waliona, walisikia na waliandika. Utamwamini nani?

## Ni kweli Yesu alifufuka toka katika Wafu?

Mashahidi wa macho kwa Yesu Kristo kwa kweli walizungumza na walitenda kama walivyoamini, alifufuka toka katika wafu baada ya kusulubiwa kwake. Ikiwa walikosea basi uKristu umeanzishwa kwa uongo? Lakini kama walikuwa sahihi, muujiza huo ungethibitisha yote Yesu aliyosema kuhusu Mungu, kuhusu yeye na kutuhusu sisi.

Lakini ni lazima tuamini ufufuko wa Yesu Kristo kwa imani pekee, au kuna ushahidi wowote wa kihistoria? Wakosoaji kadhaa walianza uchunguzi kwenye kumbukumbu za kihistoria kujaribu kuona kama kweli maelezo ya ufufuko yalikuwa uongo. Kitu gani waligundua?

Kuangalia ushuhuda wa madai makuu yaliyowahi kufanyika ya ufufuko wa Yesu Kristo!

Bonyeza hapa kwa ajili ya kudai zaidi fantastic milele alifanya – ya ufufuo wa Yesu Kristo!